

# »Dalili za ng'ombe mgonjwa«

Hata ng'ombe wanaozalishwa zaidi hawatazalisha kama inavyotarajiwa wanapokuwa wagonjwa, kwa hivyo ni muhimu kutunza afya ya mnyama.

Mnyama mwenye afya atakuwa na kiwango cha halijoto kati ya digrii 38 na 39, sauti ya kawaida ya mapafu, kupumua na sauti. Mnyama mwenye afya anapaswa pia kuwa na manyoya nyororo, hamu ya chakula na maji, kinyesi cha kawaida, rangi ya kawaida ya mkojo, na lazima awe na wanyama wengine kila wakati na sio kujitenga.

## Dalili za afya mbaya

Wanyama wagonjwa hawana hamu ya kula yaani mnyama hali kabisa wala kunywa, na huwa na manyoya magumu.

Huwa na uzalishaji duni, yaani, uzalishaji wa maziwa hupungua, mnyama huanza kujitenga na hubaki nyuma wakati wanyama wanatembea katika kikundi.

Wanyama wagonjwa pia wana mdomo mkavu, na mara nyingi wana matatizo katika umeng'enyaji wa chakula, jambo ambalo husababisha kuhara au kushindwa kupitisha kinyesi.

Mnyama hukohoa na kushindwa kupumua iwapo ugonjwa umeathiri mfumo wa kupumua.

## Utambuzi wa wanyama wagonjwa

Unapoona kwamba mnyama ni mgonjwa, uliza kuhusu historia ya ugonjwa huo kwa mfano ulianza lini na kwa muda gani mnyama amekuwa nao. Fanya ukaguzi wa jumla ambao unaweza kuangalia mazingira, sauti ya moyo na mapafu.

Baada ya ukaguzi wa jumla, fanya utambuzi tofauti ambapo unataja sababu zote zinazoweza kuleta hali hi ya ugonjwa huo.

Baada ya hayo, fanya ukaguzi maalum ambao sasa unabaki na ugonjwa maalum tu unaoathiri ng'ombe na uanze kuutibu.

Ikiwa huna uhakika wa ugonjwa maalum, rejea kwa daktari wa mifugo.